ilivyoharibika. (Picha na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa).

# RC Tabora atoa wiki 2 kubadili mazingira ya machinjio

**Na Mwandishi Maalumu, Tabora**

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Balozi Dk Batilda Buriani ametoa wiki mbili kwa uongozi wa Manispaa ya Tabora kukarabati na kusafisha Machinjio ya Ng'ombe ya Kariakoo ili kuweka mazingira mazuri ya utoaji wa huduma.

Dk Batilda alisema hali ya usafi katika eneo hilo hauridhishi na kuongeza ndani ya kipindi hicho uchafu wote yakiwemo maji yanatokana na usafishaji nyama ndani ya machinjio yaelekezwe sehemu stahili.

Alitoa kauli hiyo wakati wa ziara yake ya siku moja ya kukagua machinjio ya Kariakoo ambayo ndio yanatoa huduma ya uchinjaji wa ng'ombe , mbuzi na kondoo kwa ajili ya mboga za wakazi wa Manispaa ya Tabora na maeneo ya jirani.

Alisema manispaa ya Tabora wahakikishe wanaweka marumaru kwenye sakafu na kupiga rangi wakati wakisubiri kujenga mradi mkubwa wa kimkati wa machijio ya kisasa.



Dk Batilda alisema sanjari na hilo ni vema wakaboresha ukaushaji wa ngozi ili kuziongezea thamani kuliko ilivyo hivi sasa ambapo zinawekwa kwenye udongo wakati wa ukaushaji.

Aidha alisema uboreshaji wa machinjio hayo utasaidia kutoa huduma nzuri kwa wateja na mapato ya halmashauri yataongeza kutokana na tozo wanatoza.

Mkuu wa Wilaya ya Tabora, Dk Yahya Nawanda alisema watajitahidi kutumia fedha za ndani kukarabati maeneo yote yaliyochakaa na kufanya usafi.

Alisema ndani ya wiki mbili watakamilisha taarifa kwa mkuu wa mkoa kuhusu maendeleo ya kazi hiyo.

Awali Mkurugenzi Mtendaji, Bosco Ndunguru alisema machinjio hiyo inaweza wa kuchinja ng'ombe 80 kwa siku.

Scanned with CamScanner

FURSA ZA KIUCHUMI

# Machinjio Vingunguti na hali halisi ilivyo-3

RIPOTI MAALUMU

Mariam Mbwana, Mwananchi
mmbwana@mwananchi.co.tz





Muuzaji wa nyama akipima katika mizani kwa ajili ya kuuzwa kwa wateja katika machinjio ya Vingunguti jijini Dar es Salaam. **Picha na Sunday George**

Dar es Salaam. Nje kidogo ya lango kuu la kuingilia ndani ya machinjio utapishana na watu wengi wa kila rika, hasa nyakati za alfajiri, kwani baadhi ya watu huwa katika harakati za kwenda kazini na wengine hukimbilia hapa kujipatia mahitaji yao ya kitoweo.

Unapoingia ndani ya lango hilo utakutana na umati wa watu. Ni vigumu hata kukisia idadi yao. Wengi wakiwa wabeba mapande ya nyama kwenye mifuko au vyombo vya plastiki kama ndoo.

Kwa wale wanye usafiri hufika na magari yao ili kuwarahisishia usafiri wakati wa kurejea walipotoka. Asilimia kubwa wakiwa ni wafanyabiashara wa nyama katika mabucha mbalimbali mjini pamoja na wafanyabiashara wanaojishughulisha na uuzaji wa vyakula.

Nazidi kuingia ndani kwenye machinjio. Chini kwenye sakafu kumetapakaa damu, harufu kali inayosababishwa na shughuli za uchinjaji.

Huku nako nakutana na wauza nyama pamoja na wachinjaji wakiwa wamevalia makoti meupe yenye madoa ya damu kutokana na shughuli za uchinjaji na ubebaji wa nyama kutoka sehemu moja hadi nyingine mithili ya madaktari.

Nyama hizo hutolewa ndani ya machinjio na kuwekwa nje ambako hutundikwa kabla ya kuuzwa kwa mamia ya wateja wanaofika hapa kila siku.

Nakutana na mwanamke mmoja anayejitambulisha kwa jina la Shukuru Ezekieli, ambaye anajishugulisha na uuzaji wa nyama ya n'gombe na mbuzi anayesema wanyama wanaochinjwa katika machinjio hayo wengi hununuliwa kutoka mnada wa Pugu.

Pembeni ya machinjio hayo nakutana na jengo jipya la kisasa ambalo limebeba matumaini makubwa kwa wakazi wa eneo la Vingunguti ambalo hata hivyo, ujenzi wake bado haujakamilika ili kuipa jamii hiyo machinjio ya kisasa.

Haya ni machinjio mapya ya kisasa yanayotarajiwa kuanza kufanya kazi hivi karibuni, ujenzi wake ukikamilika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipofanya ziara katika eneo hilo Mei 17, Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Jumanne Shauri alisema machinjio hayo mapya yatakapoanza kufanya kazi yataongeza ufanisi katika shughuli za uchinjaji na kuboresha mazao yatokanayo na wanyama wachinjwao, kwani kutakuwa na mashine za kisasa.

"Machinjio haya ya kisasa yatakapoanza kufanya kazi yataongeza thamani ya nyama na vitu vingine vitokanavyo na wanyama wachinjwao hapa, hivyo kuongezeka kwa soko la ndani na nje ya nchi," alisema Shauri.

Pia yatawezesha ajira zaidi ya 3,000 hivyo kupunguza idadi ya vijana wasio na ajira mtaani ambao watachangia uchumi wa Taifa.

### Usalama wa eneo

Veronica Yohana, ambaye ni kati ya wakazi wa eneo hilo anasema matukio ya wizi yameanza kurudi kwa kasi, hasa nyakati za asubuhi na usiku ukilinganisha na kipindi cha nyuma kidogo ambapo yalipungua kabisa.

"Wizi kwa kipindi hiki umerudi kwa kasi ukilinganisha na hapo awali. Sasa hivi watu huporwa vitu vyao asubuhi na mara nyingine hutoboa madirisha na kuiba nyakati za usiku," alisema Veronica, ambaye ni mama wa familia.

Naye Zainabu Mfaume alikiri kuwapo kwa matukio ya wizi katika eneo hilo, lakini alisema wizi unaofanyika maeneo hayo mara nyingi hufanywa na watu kutoka mbali ya eneo hilo.

"Kweli wizi unafanyika, lakini mara nyingi na watu wanaotoka mbali na eneo hili," alisema Zainabu.



Mfanyabiashara katika Soko la Vingunguti jijini Dar es Salaam akiwakusanya mbuzi anaowauza. **Picha ya Maktaba**

### Harufu

Veronica alisema harufu ya eneo hilo inawapa kero, hasa kipindi cha mvua inakuwa kali na kuwapa hofu juu ya afya zao.

"Harufu huwa kali, hasa kipindi cha mvua ambapo harufu huwa kali kiasi kwamba tunahisi tunavuta hewa chafu, hivyo kutia hofu juu ya afya zetu," anaeleza Veronica, ambaye ni mkazi wa eneo hilo kwa muda mrefu.

Zainabu anaungana na Veronika kuhusu harufu hiyo ambayo anasema imekuwa kero, lakini wameizoea kutokana na kukaa maeneo hayo kwa muda.

"Harufu ni kero, lakini tumeizoea kwa kuwa ni ya muda mrefu, pia sehemu ambayo ni chanzo cha harufu ni sehemu ambayo wafanyabishara wa damu wanapata riziki yao," anasema Zainab, mama wa watoto watatu.

### Changamoto zilizopo

Baadhi ya wafanyabiashara wa eneo hilo hawakusita kubainisha changamoto zilizopo katika biashara hiyo, huku wakiiambia *Mwananchi* kuwa changamoto kubwa wanayokumbana nayo ni ukosefu wa soko rasmi la kuuza bidhaa zao, kwani eneo hilo lina machinjio pekee.

Andrea John, ambaye ni mjasiriamali anayejishughulisha na uuzaji wa makongoro alisema wakipata soko rasmi la kuuza bidhaa zao itakuwa vizuri kwa sababu litaongeza thamani ya kipato wanachokipata ukilinganisha na sasa.

"Sisi kama wafanyabiashara tunaiomba Serikali itutengee sehemu maalumu ya kuuzia biashara kwa uhuru, ili kuepuka kukaa kandokando ya barabara na sehemu hatarishi kwa afya zetu, jambo litakaloongeza thamani ya biashara zetu," amesema Andrea, baba wa familia.

Kiongozi wa wafanyabiashara katika machinjio hayo, Joel Meshack anasema bado ujenzi wa eneo la mabucha kwa ajili ya kuuza nyama unaendelea na tayari mkurugenzi wa jiji ameagiza kukamilishwa kwa ujenzi huo

"Ujenzi wa mabucha yatakayotumika kuuzia nyama bado unaendelea na mkurugenzi ameshatoa agizo kwa wahusika kukamilisha ujenzi kabla ya kuanza kufanya ka[z] kwa machinjio mapya," anasem[a] Meshack na kuongeza:

"Kutokana na ufinyu wa en[eo] wataanza wauzaji wa nyama ku[tu]mia mabucha hayo huku utarat[ibu] mwingine ukiandaliwa."

Mkurugenzi wa Jiji la Dar [es] Salaam, Jumanne Shauri alip[o]asiliana na gazeti hili kwa nji[a ya] simu alisema ujenzi wa mab[ucha] ya kuuzia nyama unaendele[a na] yanatarajiwa kukamilika hivi [kari]buni.

"Kuhusu suala la soko [kwa] sasa ujenzi wa mabucha kw[a ajili] ya kuuzia nyama unaende[lea na] unatarajia kukamilika hivi [karibu]ni," alisema Shauri.

**02**

**Nafasi ya Tanzania barani Afrika kwa wingi wa mifugo. Inazidiwa na Ethiopia pekee.**

**MKAKATI WA KWENDA KIMATAIFA**

Kutokana na idadi kubwa ya mifugo iliyonayo, Tanzania inajifunza kwa mataifa yaliyoendelea ili ipate fursa ya kuuza nyama kwenye masoko ya kimataifa. Kusini mwa Jangwa la Sahara, Botswana ni kati ya mataifa yanayopeleka nyama Ulaya na Amerika, licha ya kuwa na idadi ndogo ya mifugo. Hivi karibuni, nchi hiyo ilikubali kuipa Tanzania uzoefu wa kuuza nyama nje.

***Kuyajua mengi zaidi machinjio ya Vingunguti, nasi tena simulizi hii ita[en]delea kesho...***

Scanned with CamScanner

# ARUA, SMS

ada ya kufanikiwa ni kunyamaza kuhusu

na mwanafalsafa kutoka Marekani.

rona

lhi ya map-

esha uwazi
ambo hili,
ananchi ili
a huu ulio-

wasiende
i ni vema
a na coro-
i iliyopita

akiweka
la tatu la
iza ugon-
na dawa

naaskofu
ni Dar es
wa Cov-
washiriki
a tahad-

i wa dini
nongeza
liokuwa

kini na
a kutu-
ni wao
anayo-

jirudia
corona
wake

UVUVI



## Hakuna jengo la wavuvi walilopewa wafanyabiashara wa Soko la Feri

**Mhariri,**

Rejea gazeti lako la Juni 24 mwaka huu katika ukurasa huu wa barua za wasomaji. Kulikuwa na barua ya malalamiko juu ya wavuvi kunyanyaswa soko la samaki Feri (zone 8A), kuchukuliwa eneo lao na jengo la ofisi ya wavuvi kupewa wafanyabiashara.

Ukweli ni kwamba, Juni 3, 2019 aliyekuwa Rais, hayati John Magufuli alitembelea Soko la samaki Feri.

Pamoja na mambo mengine, aliagiza baba na mama lishe waliopo eneo la wavuvi, yaani zone 8A, wajengewe majengo mawili ya kuuzia chakula, agizo ambalo limetekelezwa.

Pia, aliagiza wavuvi wajengewe ofisi na ukumbi wa kupumzikia na kufanya mikutano yao. Agizo hilo limetekelezwa na viongozi wa wavuvi walikabidhiwa na hadi sasa jengo hilo linatumiwa na wavuvi.

Kwa maelezo hapo juu, hakuna jengo wala eneo ambalo wamepewa wafanyabiashara.

**Imetolewa na uongozi wa soko, la samaki Feri**

SMS

Scanned with CamScanner